**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Upembezwaji wa Mwanamke kama Kihunzi cha Ufanisi wa Ujenzi wa Ujitambuzinafsia Katika Baadhi ya Bunilizi za Clara Momanyi

*Dkt. Kawira Kamwara, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Nairobi, S. L. P. 30197 – 00100, Nairobi - Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: rosekawira@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*10 Juni 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Ujitambuzinafsia, Upembezwaji, Ubaada Wa Ufeministi Wa Kiafrika, Bunilizi.*

**IKISIRI**

Jamii nyingi za Kiafrika ni za kuumeni na humpembeza mwanamke kwa kumweka katika ngazi za chini akilinganishwa na mwanamume. Upembezwaji wa mwanamke katika tungo za kifasihi na katika maendeleo ya jamii ni matokeo ya mwingiliano wa fahamu tambuzi na fahamu bwete za mtunzi hasa kwa mujibu wa utamaduni wa jamii lengwa. Mwingiliano huu wa ufahamu tambuzi na ufahamu bwete unaekezwa kwa makusudi katika utunzi wa tungo mahususi kama ilivyo kwenye tungo za Momanyi 'Ngome ya Nafsi' katika Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004), Tumaini (2006) na Nakuruto (2010). Nadharia tuliyotumia ni ya Ubaada wa Ufeministi wa Kiafrika iliyoasisiwa na Steady (1981). Mwanaufeministi huyu alisema kuwa Ubaada wa Ufeministi wa Kiafrika huweka masuala pamoja ya kijinsia, ubaguzi, mielekeo ya kiutamaduni na tabaka ili kumwangalia mwanamke kama kiumbe mtegamewa bali sio mtegemezi. Data ya usomi huu ilitokana na usomaji wa bunilizi hizi maktabani. Tuliweza vilevile kutumia mitandao kurutubisha utafiti wetu. Hivyo, ni kwa jinsi gani ambavyo utamaduni unatinga ufanisi wa mwanamke kisanii katika jamii? Ni mikakati ipi ambayo jamii imeweka kupigania ufanisi wa mwanamke? Mwanamke anachangia vipi upembezwaji wa kijinsia? Maswali haya ndiyo tulipania kuyajibu katika Makala haya.

**APA CITATION**

Kamwara, K. (2024). Upembezwaji wa Mwanamke kama Kihunzi cha Ufanisi wa Ujenzi wa Ujitambuzinafsia Katika Baadhi ya Bunilizi za Clara Momanyi. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 283-296. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978.

**CHICAGO CITATION**

Kamwara, Kawira. 2024. "Upembezwaji wa Mwanamke kama Kihunzi cha Ufanisi wa Ujenzi wa Ujitambuzinafsia Katika Baadhi ya Bunilizi za Clara Momanyi". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 283-296. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978.

**HARVARD CITATION**

Kamwara, K. (2024) "Upembezwaji wa Mwanamke kama Kihunzi cha Ufanisi wa Ujenzi wa Ujitambuzinafsia Katika Baadhi ya Bunilizi za Clara Momanyi", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 283-296. doi: 10.37284/jammk.7.1.1978

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

**IEEE CITATION**

K. Kamwara "Upembezwaji wa Mwanamke kama Kihunzi cha Ufanisi wa Ujenzi wa Ujitambuzinafsia Katika Baadhi ya Bunilizi za Clara Momanyi", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 283-296, May. 2024.

**MLA CITATION**

Kamwara, Kawira. "Upembezwaji wa Mwanamke kama Kihunzi cha Ufanisi wa Ujenzi wa Ujitambuzinafsia Katika Baadhi ya Bunilizi za Clara Momanyi". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, May. 2024, pp. 283-296, doi:10.37284/jammk.7.1.1978.

## UTANGULIZI

Kwa muda mrefu sasa tahakiki na tafiti nyingi za masuala ya jinsia katika fasihi ya Kiswahili zimekuwa zinakariri kauli na malalamiko yale yale ya mwanamke. Miongoni mwa tuhuma hizi ni kubaguliwa, kuonewa, kudhalilishwa, kukandamizwa na kupembezwa, miongoni mwa kauli nyingine sawia na hizo. Katika tungo nyingi zinazotumiwa kama vyanzo vya data na vivyo hivyo tafiti nyingi zinazoendelezwa kwa misingi ya data hizo, wanawake hawawasilishwi kama watu walio na uwezo wa kuasisi, kupanga na kutekeleza vipaumbele vyao. Kwa mujibu wa Swaleh (2011), wanawake hawasilishwi kama watu walio na ajenda mahususi, misimamo thabiti na walio wabunifu katika kutafuta suluhu za matatizo yao.

Isitoshe, hawawasilishwi kama mawakala wa mageuzi na watoaji maamuzi kwa mujibu wa miktadha mahususi ya maisha yao. Kwa kiasi kikubwa, imekuwa ada katika tafiti hizi kwa mwanamke kuwasilishwa kama kiumbe mtendwa, mhasiriwa, mtu wa kusikitikiwa na kuhurumiwa kwa kila hali. Jambo hili linaashiria mwachano ulioko kati ya usomi na hali halisi za maisha ya mwanamke. Chesaina (1989) anadai kuwa hali hii inashurutisha haja ya kutambua uanuwai wa usawa wa kijinsia, ufahamu mchungu kuwa usawa huo si kitu cha kutwaliwa na kelele za kiharakati Licha ya vihunzi vilivyopo, ni sharti kuwepo na juhudi endelevu za kuafikia usawa huo. Iwapo ataweza kuafikia upeo wa maisha yake, lazima kwanza kutambua kwamba anakandamizwa hivyo kupigania uhuru na usawa wake. Tunaweza kusema kuwa, binadamu huyu anayeitambua nafsi yake, ni yule aliye huru kuutazama uhalisi na ukweli kwa jinsi ulivyo. Mfano wa binadamu kama huyu ni mwanamke aliye na uwezo wa kuutazama uhalisi wa maisha yake.

Mbali na hayo, binadamu aliyejitambua ni mwenye uwezo wa kuridhika na kuikubali nafsi yake, nafsi ya wengine na maumbile yake kwa jinsi yalivyo na jinsi nafsi hizo zilivyo. Hufanya hivyo bila kijali kuwepo kwa kasoro, udhalili na walakini wa kimaumbile au kijamii na kihali. Ujitambuzinafsia hudhihirika kupitia uwezo wa kujitegemea pasina kuwatweza wengine wanaojaribu kujitegemea. Mogere (2003) anafafanua kuwa hali hii humfanya kuwa na ujasiri wa kutumia tajriba yake ya maisha kufanya maamuzi yake. Maamuzi hayo hayashawishiwi au kuathiriwa na mifanyiko ya kitamaduni na kimazingira. Binadamu huyu anatumia uhuru wake wa kimawazo kujenga maoni, mitazamo au hata chukulizi za ulimwengu wake. Kupitia hiari ya kujianzishia maamuzi yake mwenyewe, huwa mkweli na hivyo, anajiepusha na kujitambua kwa misingi ya kujilinganisha na wengine.

Fauka ya hayo, binadamu huyu ni aliye na malengo mahususi anayotaka kuyatekeleza kwa manufaa ya kibinafsi na waliomo katika upeo wa maisha yake. Ni kiumbe aliye na nafasi na fursa za kujitawala kwa kila hali, aliye mbunifu, asiye mtegemezi wa mamlaka au watu walio nje ya upeo wake. Ana ukunjufu wa kujiibua upya kadri ya mabadiliko ya hali za maisha yake. Binadamu anayetambua sio tu uwepo wa mahusiano bali pia umuhimu wa mahusiano hayo katika kujitambua kwa hali mbalimbali. Mwenyewe anajitambua na kuhusika kuendeleza ubinadamu wake—hisia za kijamii, umuhimu wa jumuiya. Kauli hizi za kisaikolojia na kinadharia zina maana kwamba tunataka kubainisha ni kwa jinsi na kwa kiasi gani Clara Momanyi anamjenga na kumsawiri mhusika mwanamke anayeakisi binadamu kielelezo na siyo binadamu wa kiutopia na wa ndotoni.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Hapana shaka kwamba, suala la udhalilishwaji na upembezwaji wa mwanamke katika tungo za kinathari katika fasihi ya Kiswahili limewahi kujitokeza katika tafiti za aina mbalimbali. Hivyo basi, mapitio ya maandishi na machapisho yanayojumuishwa hapa ni mapitio yaliyo na mlandano wa masuala ya jinsia pamoja na yanayomhusu mwanamke katika miktadha ya kiutunzi na kiutafiti. Mitazamo ya kijumla ya kiusomi iliyoko kuhusiana na usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili inaelekea kuafikiana kwamba, mwanamke hasawiriwi kwa njia zinazoridhisha. Miongoni mwa wasomi walioshughulikia suala hili katika misingi ya kutokuwa na usawiri wa kuridhisha ni pamoja na Chesaina (1987), Lugano (1989), Muindi (1990), Mule (1991), Momanyi (1998), Swaleh (2011) na Musyoka (2011). Kauli ya kijumla inayojitokeza katika tafiti hizi zote ni kwamba, mwanamke ni mhasiriwa, mwanamke ni kiumbe mtendwa na si kiumbe mtendaji katika ujenzi wa ujitambuzinafsia wake.

Moja kati ya masuala ya kimsingi ambayo yamewahi kutafitiwa, ni suala la umuhimu wa ushirikishwaji wa mwanamke katika michakato ya utunzi wa fasihi. Chesaina (1987) anahoji kwamba, tamthilia kama sanaa halisi ya kiutendaji ni kielelezo bora cha usawiri hasi wa mitazamo na misimamo ya mwanamume pamoja na udhalimu wake dhidi ya mwanamke. Kwa hivyo, Chesaina anaukashifu usawiri hasi ambapo anahoji na kutoa kauli kwamba ujitambuzinafsia wa jinsia kuwa ni ujitambuzinafsia unaompembeza mwanamke.Usawiri huo ndio unawezesha kuona kama mhusika anashika majukumu ya kimsingi katika jamii au kama anashika majukumu ya pembeni ambayo hatimaye, yanachukuliwa kama ithibati ya upembezwaji wake.

Suala la ujitambuzinafsia hasi au ujitambuzinafsia duni wa kijinsia ni suala linalojitokeza kwa njia nyingi mbadala katika tafiti za fasihi andishi ya Kiswahili. Kwa mfano, Lugano (1989) katika kuliangazia suala la usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya za Kezilahabi anahoji kwamba, mwanamke amesawiriwa kuwa ni kiumbe duni chini ya utawala na uelekezi wa mwanamume. Hivyo, mwanamke anachorwa au kusawiriwa kama kiumbe anayemtegemea mwanamume, japo katika kulikuza suala la utegemezi, Lugano hawasilishi ithibati inayoonyesha kwamba wanawake wasiowategemea wanaume wanafanikiwa zaidi katika mambo yao. Kwa hivyo, unadhihirisha ujenzi wa unyonge kama wasifu wa mwanamke. Hapa panaibuka mahusiano ya kiuwezo na kiunyonge. Mahusiano kama haya, ndiyo yanayotumika kama kigezo cha kuamua palipo na kipaumbele na palipo na upembezwaji.

Kauli hizi za Lugano zinawiana na kauli za Muindi (1990), ambaye anadai kwamba ubaguzi wa kijinsia unaibua hali ya mwanamke kupembezwa kwa kutazamwa kama kiumbe duni katika jamii. Kwa kumwangalia mwanamke katika miktadha ya ukahaba, Muindi anahoji kuwa umaskini unamsukuma mwanamke hadi kwenye ukahaba kwa sababu nyenzo za uzalishaji mali zinadhibitiwa na jinsia ya kiume. Haya ni mambo ambayo Momanyi ameyashaghulikia kwa njia kadha wa kadha. Kwa kuwa Lugano na Muindi wamesukumwa na mitazamo tofauti ya kinadharia, makala haya yalitaka kubaini ni kwa kiasi gani mitazamo ya kimakuzi, kiitikadi na kinadharia ya Momanyi imeshirikishwa katika usawiri wake wa wahusika.

Suala la upembezwaji wa mwanamke linabainika katika tanzu za fasihi simulizi kupitia msukumo wa kuukeni au kuumeni. Kupitia kwa utanzu wa methali mwanamke anazidi kupembezwa kupitia kwa matumizi ya lugha ya kitamathali katika jamii husika. Baadhi ya methali humpembeza mwanamke na kumpa utambuzinafsia hasi kama anavyohoji Ndungo (1998) katika tasnifu yake ya Uzamifu. Mila na desturi ni baadhi ya vigezo vinavyoisimamisha jamii kama asasi muhimu kupitia kanuni zilizowekewa wanawake kwa wanaume kwa mujibu wa mielekeo ya kijamii. Aidha, wanawake hasa wale walioelewa vijijini wanapembezwa kwa kupewa ujitambuzinafsia hasi kwa kutazamwa kama washenzi, wategemezi wa wanaume na wakosa mwelekeo katika maisha. Kwa mujibu wa mila na desturi za jamii

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

anazolenga Ndungo (1998), mwanamume anahusishwa na hekima ya kuielekeza jamii na hivyo, kumjengea ujitambuzinafsia chanya huku ujitambuzinafsia wa mwanamke ukidunishwa. Tuliweza kubaini kuwa Momanyi ana mwelekeo sawia na hoja za Ndungo (1998) katika kumpembeza mwanamke.

Swaleh (2011) anasema kuwa ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia umeathiriwa pakubwa na utamaduni, mfumo wa ubabedume pamoja na mazingira anamokulia mwanajamii. Vigezo vya utamaduni na mazingira vimekuwa kikwazo katika kujenga ujitambuzinafsia wa jinsia katika jamii za watunzi wa bunilizi teule alizochanganua. Ni mtazamo mwafaka uliotuelekeza katika kuchunguza ikiwa mtunzi Clara Momanyi anaathirika sawia katika kuangazia vihunzi vya utamaduni vinavyoathiri ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia na upembezwaji wa mwanamke katika tungo zake.

## MISINGI YA KINADHARIA

Katika makala hii, tumeongozwa na nadharia ya Ubaada wa Usasa wa Ufeministi. Nadharia hii imezaliwa na nadharia ya Ufeministi kupitia mabadiliko ya kimtazamo kumhusu mwanamke katika jamii. Nadharia hii imeteuliwa kwa misingi kwamba Ubaada wa Usasa wa Ufeministi una madai, kanuni na mwelekeo wa kiusomi unaowiana na masuala yanayojadiliwa katika kazi hii. Wamitila (2002) anasema kuwanadharia hii hulenga kujadili, kubainisha na kupendekeza misimamo ya uelewa, michakato ya uchanganuzi na mikakati ya utatuzi wa itikadi zinazomkwamisha mwanamke. Aidha, michakato na mikakati inayodhamiria kuweka wazi na kutetea haki za wanawake dhidi ya ubaguzi wa kijinsia. Ubaguzi huu unasababishwa na mitazamo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na kidini. Nadharia ya Ubaada wa Usasa wa Ufeministi inayoweza kutumika kiutekelezi inahitaji kwanza pawepo fikra za kukiri kwamba bara la Afrika halina mfumo mmoja tu wa utamaduni. Badala yake lina uchangamano endelevu wa kiutamaduni unaochangia kuibuka kwa uelewa changamano wa suala zima la jinsia, dhana ya jinsia na vilevile falsafa changamano za jinsia.

Mikell (1997), anadai Ubaada wa Usasa wa Ufeministi kwa kujikita kwenye bara la Afrika, unatofautiana na Ufeministi wa kimagharibi kwa misingi kwamba unaweka kipaumbele katika masuala ya upatikanaji na uwezo wa udhibiti wa mahitaji ya kimsingi ya maisha, masuala ambayo ni tofauti sana na masuala yanayopewa kipaumbele katika ufeministi wa kimagharibi. Kwa misingi hii, mahitaji, uhalisi, ugandamizwaji na uwezeshwaji wa wanawake wa Kiafrika ni masuala yanayoweza kushughulikiwa kihalisi. Nadharia hii inafumbata masuala ya kifeministi ya kijumla pasina kubeza, kubana au kupembeza uhalisia na upekee wa mwanamke wa Kiafrika. Kwa maoni ya Nkealah (2006), Ubaada wa Usasa wa Ufeministi kwa kujikita na bara la Afrika, unapania kuasisi kutambuliwa kwa mwanamke wa Kiafrika wa kisasa, aliye huru, mzalishaji, anayejitegemea kadri inavyowezekana katika miktadha anuwai ya tamaduni za Kiafrika.

Pinkie (2006) anaunga mkono haja ya kukubali na kujiepusha kushikilia chukulizi kwamba mwanamke wa Kiafrika anatokana na historia, utamaduni na asilia yenye kiini kimoja. Ni sharti Ubaada wa Usasa wa Ufeministi kwa kujikita kwenye bara la Afrika utambue na ujiepushe na ukariri wa kauli bubu na za kibaguzi, kauli zinazotenga badala ya kuleta pamoja, kauli zenye mtazamo finyu badala ya mtazamo mpana na jumuishi, kauli zilizo na mahusiano halisi ya kiutekelezi katika hali na miktadha ya Kiafrika ya kisasa. Kauli hii ni muhimu katika kubaini upekee wa kiutunzi wake Momanyi.

## MBINU ZA UTAFITI

### Ukusanyaji na Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Ukusanyaji data ulilenga kazi za Momanyi ‘Ngome ya Nafsi’ katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Tumaini* (2007) na *Nakuruto* (2010). Ili kuafikia lengo la makala haya, tulijihusisha na usomaji wa kazi hizi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

kwa lengo la kuchanganua upembezwaji kama kihunzi cha kujenga ujitambuzinafsia wa jinsia.

Hivyo, tulizingatia sampuli ya kimakusudi ambayo kwa kawaida humwezesha mtafiti kuamua mahali pa kupata data kulingana na madhumuni na malengo ya utafiti wake. Zaidi ya hayo, uteuzi wa kimakusudi ulituwezesha kupata matini tulizohitaji katika kazi teule za mwandishi Momanyi. Isitoshe, uteuzi wa kimakusudi ulizingatia kigezo cha jinsia ya mwandishi, vipindi kazi hizi zilipotungwa na upeo wa mitagusano na migogoro ya kijinsia katika tungo zake tatu.

Katika utafiti huu elezi, tulihusisha kufafanua namna data ilivyoteuliwa na jinsi inavyohusiana na mada yetu kwa kufungamana na nadharia ya Ubaada wa Ufeministi wa Kiafrika. Kwa kuzingatia mbinu hii, tulichanganua bunilizi teule ili kupata kujua ni kwa jinsi gani mtunzi anavyoliangazia upembezwaji kama kihunzi cha kujenga ujitambuzinafsia wa jinsia katika tungo zake alizotunga moja baada ya nyingine.

## UTAMADUNI JADI KAMA KIHUNZI CHA KUTINGA UFANISI WA MWANAMKE KATIKA 'NGOME YA NAFSI'

Ngome ya Nafsi' ni hadithi fupi kwenye diwani ya hadithi fupi ya *Mayai waziri Wa Maradhi* na *Hadithi Nyingine* (2004). Mwandishi Momanyi anamulika jamii inayojikita kwenye mila kandamizi kwa mtoto msichana. Mtoto msichana ananyimwa nafasi ya kuendeleza masomo yake kwa kuozwa angali bado mchanga. Jamii hii inazingatia mfumo jadi wa ki-ubabedume ambapo mtoto msichana anachukuliwa kama kitega uchumi. Utamaduni wa jamii hii unampa mwanamume mamlaka juu ya familia yake na hivyo, kumpa nguvu na uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu familia yake.

Momanyi amemtumia mhusika Mzee Mengo ambaye ni babake Naseko, kuonyesha ubinafsi wa mwanamume kwa kumwoza bintiye akiwa bado shuleni. Analetewa mifugo na tajiri Mzee Sakaja ambaye ni mzee wa rika lake. Utawala wa mwanamume kwa mwanamke unadhihirika pale ambapo mkewe Mengo Bi. Kija anafahamu mpango wa kuozwa kwa bintiye lakini hamtahadharishi kamwe. Kaida za kijamii zinampasa kumuunga mkono mumewe katika masuala ya kumtafutia binti yao mchumba. Mtazamo huu kwa mwanamke unamfanya Naseko kutekwa nyara na mabarobaro akitoka kuchota maji. Anajaribu kujinusuru lakini anakinzwa nguvu. Momanyi anaonyesha makali ya utamaduni jadi kwa mwanamke. Tunasoma,

> *'La hasha! Haiwezekani,' aliwaza Naseko. Alianza kulia kwa kwikwi huku akitupatupa miguu na mikono yake hewani ili kujinasua. Ilikuwa ni patashika, nguo kuchanika. Vijana hao wenye misuli iliyojaa siha, hawakushindwa kuvizuia vile vikumbo vyake. Naseko alikuwa kama mzigo wa sufu tu kwao... (uk. 100).*

Jamii inamchukulia mtoto msichana kama kiumbe dhaifu. Ananyimwa uhuru wa mawazo. Anaamuliwa mkondo wa maisha na ada za jamii yake. Kushindwa kujinasua kwa Naseko kunaonyesha kwamba bado mfumo wa Ki-Ubabedume una nguvu zaidi juu ya mwanamke. Iwapo mwanamke anajaribu kupigania uhuru wake, kwa kiasi kikubwa hushindwa nguvu na kanuni alizotengewa na jamii. Yeye ni mtawaliwa. Anachukuliwa kama mtu asiye na usemi kuhusu maisha yake. Hii ndiyo sababu mamake Bi. Kija ananyamaza na kutazama tu wakati bintiye anaponyimwa haki ya kupata elimu. Yeye kama Naseko, wanatawaliwa na mumewe na hawaruhusiwi na kaida za jamii yao kumpinga kwa vyovyote vile au jambo lolote lile.

Mwanamke ameikubali hali yake na kuruhusu nguvu za Ki-ubabedume zimtawale. Hii ndio sababu wanawake wenzake wanamkejeli Naseko anapojaribu kujinasua. Momanyi anaashiria kwamba bado jamii za Kiafrika hazijafikia kikamilifu utambuzi wa haki za mwanamke. Mikakati mingi imewekwa na watetezi wa haki za kibinadamu kumhakikishia mwanamke uhuru na haki. Inabainika kwamba bado kuna mengi yanayohitaji kutekelezwa iwapo upembezwaji wa mwanamke utakomeshwa. Ni wanawake wachache ambao wanaweza kujikomboa katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

jamii hii. Kwa mfano, mke wa tatu wa Mzee Sakaja aliaga dunia kutokana na matatizo ya uzazi. Lakini kifo cha msichana huyu hakiizindui jamii kukomesha udhalimu wa aina hii.

Mwanamke anapembezwa kupitia uzingativu wa tamaduni dhalilishaji kwa mwanamke kama vile tohara, ndoa za mapema pamoja na kunyimwa nafasi ya kupata elimu. Mwanamke naye hayuko kimya kudhalilishwa. Anajitahidi kupigania uhuru na haki yake. Kupitia kwa mhusika Naseko, inadhihirika jinsi Momanyi anavyofaulu kumjengea mwanamke matumaini ya kushinda vita dhidi ya mila na desturi dhalalishi za jamii anayoisawiri na kuiwasilisha. Mwanamke huyu amejitambua hivi kwamba hana budi kupigania hadhi yake. Hii ndiyo sababu Naseko anajaribu kutoroka kutoka nyumbani kwa Mzee Sakaja. Uwezo na mamlaka ya mwanamume katika jamii hii inatiliwa shaka. Tunasoma kwamba, alifungiwa kwenye chumba kimoja kidogo baada ya kufikishwa kwa Mzee Sakaja. Hali hii ya 'kufungiwa' inaonyesha kwamba jamii inatambua uwezo wa mwanamke wa kujikomboa lau angelipewa upenyo. Kuna mkinzano kati ya ukale na usasa kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii hii. Kizazi kipya kinapinga mila kandamizaji kama vile uchaguzi wa mchumba na ndoa za mapema. Kinatetea nafasi stahiki kwa mwanamke. Sauti ya ukombozi wa mwanamke inasikika kupitia kwa Naseko anaposema;

> *'...lazima nitoke humu kabla ya jizee lile kuingia humu tena', alijipa moyo. Alichukua kile kijimeza na kukiweka kiti juu yake. Kisha akapanda kwa hadhari juu ya kiti hicho, ...kwa uangalifu mkubwa, alishuka pale juu alipojipachika na kuzima ile taa.Alijizoa haraka na kumwaya nyayo bila kutazama nyuma... (uk. 107-108).*

Ni bayana kuwa mwanamke amekinaishwa na mfumo jadi. Mwanamke huyu anataka kufanya mageuzi, ni mwanamabadiliko anayetambua kwamba anapembezwa. Anakashifu ubinafsi wa mwanamume anayezingatia mfumo jadi. Naseko, kama mwanamke wa aina hii, anaenda kinyume na maamuzi ya babake (mwanamume) kuhusu maisha yake. Ukombozi wa Naseko unaonyesha uasi wa mila na desturi kandamizaji dhidi ya mwanamke. Kuna uwezekano wa mwanamke kujitambua na kupinga udhalilishaji dhidi yake. Kwa nini Naseko aolewe kama mke wa nne? Kwa nini atamatishe masomo yake? Kwa nini ahatarishe maisha yake? Hayuko tayari kufuata kila ada za jamii yake. Kwa hivyo, mwanamke amepiga hatua katika kutetea haki na nafasi yake katika jamii. Ingawa anatarajiwa kuzingatia utaratibu aliowekewa kikalautala, lazima akaidi amri hizo ikiwa zinahatarisha maisha yake.

Mbali na juhudi za mwanamke binafsi yake kujikomboa, wasomi na makundi ya kijamii wamezinduka katika vita dhidi ya upembezwaji wa mwanamke. Tamaduni dhalilishaji zinapigwa vita. Wanapigania hadhi ya mwanamke katika mazingira ya utawala na mfumo wa ki-ubabedume unaotiwa nguvu na utamaduni. Lengo kuu ni kupiga vita uonevu wa kiasili kwa mwanamke. Tunaona jinsi Bi. Tesi anavyopiga vita upembezwaji wa mwanamke. Anawajengea watoto wasichana makao yanayowapa mazingira mwafaka ya kuendeleza masomo na kuepuka ndoa za mapema. Kupata makao mapya kwa Naseko kunaonyesha na kuashiria hatua za jamii katika kumhakikishia uhuru na matumaini mtoto msichana. Ni bayana kwamba jamii inatambua nafasi hasi ya mwanamke na inaelekea kujaribu kuibadili. Mabadiliko haya yameendelezwa kwa kina katika bunilizi ya *Tumaini* (2007).

## Makali ya Upembezwaji wa Mwanamke katika *Tumaini* (2007)

Kupitia kwa mhusika mkuu Tumaini, inabainika jinsi mwanamke anavyopembezwa katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa Ki-ubabedume. Katika mfumo huu, mwanamume hupewa uwezo zaidi huku mwanamke akipewa nafasi finyu na kufanywa dhaifu. Mwanamke anaonyesha uwezo wake katika kupania ujitambuzinafsia wake tena kutimiza ndoto zake maishani. Anaubadilisha udhaifu anaodhaniwa na kupandikizwa na jamii yake, akaubadili kuwa uwezo wa kufanya maamuzi yake binafsi kujihusu yeye na jamii yake.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

Chini ya mfumo wa Ki-ubabedume, mwanamke anatengewa majukumu ya kulea na kutunza watoto pamoja na kuwafunza tabia njema. Mtoto msichana anastahili kuandaliwa vyema ili aweze kuwa mke na mama bora katika jamii. Hivyo, lazima apashwe tohara ili aweze kufunzwa ada za jamii kuhusu majukumu yake kulingana na sifa zake za kibiolojia. Baada ya tohara, anahitaji kuolewa ili familia yake iweze kufaidi mahari. Jamii yenye itikadi za aina hii ndiyo Momanyi analenga katika riwaya ya *Tumaini*. Makali ya utamaduni wa aina hii unamwathiri Tumaini ambaye anapangiwa tohara akiwa darasa la saba. Babake Mzee Masumbuko, hajali kuwa Tumaini bado ni mwanafuzi. Jambo la thamani kwake ni kumpasha tohara bintiye, kisha kumwoza. Taswira hii ya kijadi inamfunga pingu mtoto msichana na kumfanya aishi chini ya utumwa wa kiutamaduni. Hapewi nafasi ya kujiendeleza ila hulazimika kuzingatia ada alizowekewa na jamii tangu mwanzo.

Katika bunilizi ya *Tumaini* (2006), tunapata mkinzano mkubwa na dhahiri kati ya 'tamaduni' mbili. Kuna utamaduni wa jadi unaowakilishwa na Mzee Masumbuko ambaye ni babake Tumaini. Halikadhalika, kuna utamaduni wa kisasa unaowakilishwa na mhusika Tumaini. Kama mwakilishi wa utamaduni jadi, Mzee Masumbuko anaashiria ukosefu wa utu toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Anawakilisha uwezo za utamaduni jadi na jinsi ilivyo vigumu kuupiga vita. Kutobadilika kwa Mzee Masumbuko kunaashiria kwamba utamaduni hautapotea ilmuradi unainjikwa na mfumo wa ki-ubabedume. Lazima jamii ijifungamanishe na mila na desturi za kijadi. Mzee Masumbuko anashikilia imani yake kuwa, yeye ndiye kiongozi wa familia na hana budi kutekeleza wajibu na majukumu yake kadri utamaduni unavyotaka na kudai.

> Mbali na hayo, kuna utamaduni wa kisasa unaowakilishwa na Tumaini pamoja na familia ya Mzee Shabani. Utamaduni huu unapiga vita mila zinazochangia upembezwaji wa mwanamke zikiwemo ndoa za mapema, ukeketwaji, ubaguzi kwa misingi ya kijinsia na kibiolojia, katika maendeleo ya jamii pamoja na udhalilishwaji kingono. Mila hizi zinamzuia mwanamke kuafikia ujitambuzinafsia chanya. Mhusika Tumaini anajikuta katikakati ya mila na desturi duni za ndoa za mapema na kupashwa tohara ambazo hazimpi nafasi ya kuafikia ndoto yake ya kimasomo. Anapinga mikakati anayowekewa na jamii yake. Tunamwoa Tumaini akisimama kidete na kumwambia mamake, '*...ikiwa unayotaka kunieleza yanahusu tohara, mama sahau- sahau kabisa maana nilisema tangu kitambo kuwa mila kama hiyo ni ya kizamani, ni ya kikatili na kishenzi....*' (uk 16).

Tumaini anawakilisha kizazi cha kisasa ambacho kinajitambulisha na kuelewa haki zake. Ni kizazi ambacho hakiko tayari kuzingatia ada za mfumo jadi. Hakiko tayari kufuata ububu wa mila kandamizi na kuzima maazimio ya kushiriki kwenye maendeleo ya jamii. Kizazi hiki kimejukumika kuufasiri uhuru wake na kujua kile ambacho kinahitaji na kukipigania. Kinapiga vita ukalautala kwa kila njia iwezekanayo. Kimehamasishwa kuhusu nafasi yacho chanya katika jamii. Ni kizazi kinachofanya kila linalowezekana na kuwapo katika uwezo wacho kuhakikisha kwamba hakuna yeyote au lolote linalozima ndoto yacho. Mwanamke mwenye msimamo kama huu hupigania haki yake bila kufa moyo. Hii ndiyo sababu Tumaini anatoroka kwao nyumbani usiku wa manane ili asishirikishwe kwenye ada ya upashwaji tohara. Anatorokea kwa mamake mdogo ili angalau apate afueni na kuendeleza masomo yake.

Vita vya kupigania ujitambuzinafsia wa mwanamke havimaliziki baada ya Tumaini kutoroka nyumbani kwao. Hata akiwa kwa mamake mdogo, bado makali ya utamaduni kandamizaji yanamwandama. Babake Mzee Masumbuko anaenda Maunguja kwa rafiki yake kichinichini kumtafutia Tumaini mchumba. Wanapoleta posa, Mzee Mabruk anasema, '*...tumekuja kumposa binti yenu Tumaini...*' (uk. 61). Tunaona kuwa, mtoto msichana hapewi uhuru wa kimawazo. Makali ya utamaduni jadi yangali yanamwandama. Utamaduni unampa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

mwanamume uweo na mamlaka ya kuiamulia familia yake jinsi aonavyo sawa. Hii ndiyo sababu inayomfanya babake, Mzee Msumbuko, amnyime bintiye nafasi ya kusoma na kukomaa kiakili ili eweze kujipangia mikakati ya maisha yake ya baadaye. Ada ya ndoa ni mojapo ya upembezwaji ambao watetezi wa haki za binadamu wanapingana nao.

Katika kumjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya, jamii inajitolea kutetea haki za mtoto msichana. Ndoa za mapema zinapigwa vita vikali ili kumwezesha mtoto msichana kuendeleza masomo yake. Momanyi anaonyesha kwamba kizazi cha kisasa kinaungwa mkono na wanajamii ambao wametambua hatari za mila na desturi zinazomkandamiza mtoto msichana. Wanajamii hawa ni kama mjomba Shabani na mkewe Bi. Halima. Serikali vilevile haijaachwa nyuma kuhakikisha kwamba mtoto msichana anapata haki zake. *'...Siku hizi hakuna mtoto wa kike anayekubali kupashwa tohara..wengine hata wamewachukulia wazazi wao hatua za kisheria kuhusu jambo hili ...'* (uk. 40). Maneno ya Mzee Yusufu yanaonyesha jinsi ambavyo jamii inavyojitolea kupiga vita uonevu dhidi ya mwanamke. Jamii inajitahidi kukomesha ufifishwaji wa mamlaka kwa mtoto msichana.

Mwanamke anadhalilishwa katika nyanja nyingi za maisha. Mbali na kupembezwa katika mazingira ya nyumbani, hata mazingira ya shuleni hayamweki. Hii ina maana, ni lazima mwanamke apiganie nafasi yake bila kufa moyo. Tumaini anapopata afueni ya kutopashwa tohara na kuozwa mapema, anadunishwa shuleni na wanafunzi watundu kwa kutoroka nyumbani kwao. Isitoshe, anaandikiwa barua ya mapenzi na mwanafunzi mwenzake Sifa. Jambo hili linamkera sana Tumaini na kumfanya amshitaki Sifa kwa mwalimu wao Mwadime. Sifa anaadhibiwa. Mwanamke anayejitambua hana budi kutafuta haki yake iwapo anapembezwa. Tunaweza kusema kuwa Tumaini anatumiwa kuwafumbua macho watoto wasichana kutojihusisha na mapenzi wakiwa bado wadogo. Inaonekana kwamba Tumaini anajielewa, akayaelewa mazingira ya jamii yake na ndipo anachukua tahadhari dhidi ya mambo yanayoweza kuhatarisha maisha yake.

Kama asemavyo Mavisi (2007), kuna visa vingi vya watoto wasichana wanaopata mimba za mapema hasa wa shule za msingi. Wanadanganywa na wavulana na kuachwa wajawazito. Masomo yao yanakatizwa na hapo huwa wanakosa uwezo wa kujijenga kimaisha. Hili linakuwa tisho kwa ujitambuzi wa mwanamke katika jamii. Kinyume na hali kama hii, tunaweza kusema kuwa ujasiri wa Tumaini wa kumshtaki Sifa unaonyesha kwamba yeye ni msichana anayejitambua. Anajiheshimu na hivyo, hataki kuchezewa na mtu yeyote. Tumaini anapinga udhalimu dhidi yake kwa kudhihirisha ushujaa ambao unaweza kuigwa na watoto wasichana wanaokumbwa na hali sawia na yake. Amefahamu kuwa njia mbili zilimshinda fisi. Hivyo, anashika njia ya masomo huku akifahamu kuwa mapenzi yatakuja baadaye.

Jamii imekuwa ikimkandamiza mwanamke kwa kumnyima sauti ya kujieleza au kupinga mambo yanayomuumiza moyoni. Ukandamizwaji huu hupigwa vita na watetezi wa haki za binadamu. Mwanamke amehamasishwa kutetea haki yake. Tunamwona Tumaini akivamia kikao cha kamati ya ufadhili wa wanafunzi wanaohitaji ufadhil ili kupata haki yake. Hii ni baada ya babake kumwendea kinyume na kuhakikisha jina lake limeondolewa kwenye orodha ya wafadhiliwa. Babake analipiza kisasi baada ya Tumaini kushinda vita dhidi ya ukandamizwaji kutoka kwake. Kwanza anatoroka asije akapashwa tohara kishaa kuolewa. Ushindi wa Tumaini unakuwa kero kwa babake. Kama kiongozi wa familia, anahisi mamlaka yake yameingia doa na kwamba anadhalilishwa. Mzee Masumbuko anaonyesha katawaliwa na taasubi ya kiume na mfumo wa ubabedume kwa kuhakikisha Tumaini amenyimwa ufadhili. Mzee Masumbuko anakosa kutambua uwezo wa Tumaini wa kupigania haki yake.

Momanyi amefaulu katika kuonyesha kwamba kizazi kipya ni tofauti na kizazi cha jadi ambapo mwanamke hakuwa na usemi mbele ya mwanamume. *'....Hakujali hatua ambayo*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

*ingechukuliwa na wahusika wa mkutano huo...*' (uk. 98) . Mwanamke yuko radhi na tayari kupigania haki yake kwa vyovyote vile. Kule kuvamia kikao cha tarafa cha ugavi wa pesa za ufadhili kwa watoto maskini, kunaonyesha jinsi wakati ulivyopita wa mwanamke kupembezwa kimasomo... '*ingechukuliwa na wahusika wa mkutano huo...*' (uk. 97-98). Mwanamke hana budi kujitambua na kuhakikisha kwamba anafaidika sawia na mwanamume. Haya ni miongoni mwa mabadiliko chanya katika asasi za kijamii katika kukuza na kutekeleza haki sawa kwa jinsia mbili. Tunaona kwamba baada ya tukio hilo Tumaini anapata kugharamiwa masomo ya sekondari.

Katika jitihada za kupinga usaguzi, mwanamke anakumbana na changamoto za kuchukuliwa kama chombo cha kutimiza uchu wa mwanamume wa kimapenzi. Anaposhindwa nguvu na mwanamume, hujikuta na mimba nje ya ndoa au maradhi ya zinaa. Tunaona hali hii pale ambapo Chifu Andrea anajaribu kumbaka Tumaini. Kwa bahati nzuri, Tumaini anatumia akili yake na ujanja kujinusuru. Tunapata taswira ya kiumbe aliyepevuka na kupata ujuzi wa kujikinga dhidi ya hatari zinazoweza kuyaathiri maisha yake. Kupitia kwa unyama wa Chifu Andrea tunapata kuelewa na kufahamu jinsi jamii ilivyochujuka kimaadili. Imejawa na ubinafsi na uhayawani ambao unaifanya kuyadhuru maisha ya mtoto msichana. Ni wasichana wachache wanaoweza kujinasua kama anavyofanya Tumaini. Wengine hushindwa kabisa na hivyo, kuhatarisha maisha yao.

Mbali na unyama wa Chifu Andrea, mwanawe Majuto vilevile anajaribu kumbaka Tumaini. Si jambo jipya linalomwandama mtoto msichana katika jamii. Kumekuwa na visa ambapo baba na mwanawe wa kiume wanashiriki ngono na msichana mmoja. Ni swala analolirejelea Mohammed (1980) wakati ambapo Maksuudi na mwanawe Mussa, wanakuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kazija (uk. 13-15). Tabia kama hii inaonyesha wazi jinsi kizazi hiki kinavyojiangamiza chenyewe. Badala ya Chifu Andrea kumpa mtoto msichana nafasi ya kukua na kuwajibika katika jamii, anakusudia kumchafua.kwa upande mwingine. Jamii imefaulu kwa kiasi fulani kumwandaa mtoto msichana kujinasua pindi anapokabiliwa na jaribio la ubakaji ndipo "*...Tumaini anampiga Majuto kwa kiko cha mkono sehemu ya kinena kwa nguvu zake zote ...*" (uk. 89).

Mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu kimasomo. Iwapo ana uwezo sawa na mwanamume, jamii inampembeza. Amekuwa akihusishwa na majukumu yasiyohita ujuzi wa juu au wa kitaaluma akilinganishwa na mwanamume. Mtazamo huu hasi kwa mwanamke ndio unaitawala akili na mtazamo wa mwalimu Majaaliwa anapomzuia Tumaini kujaza kosi za sayansi za chuo kikuu... '*Nyie wasichana ni vigumu sana kufuzu katika masomo haya.'... 'Mwalimu liwe liwalo, mimi nataka kuchagua masomo ya sayansi kwani najiamini kwamba nitafaulu...*' (uk 115-116). Mwanamke anajiamini kama tumwonavyo Tumaini akifaulu vyema kwenye masomo ya sayansi. Anaamini kwamba ndiye pekee mwamuzi wa maisha yake kama asemavyo; '*...I want to shape my destiny*' (uk 136). Kutofaulu kwa Mwalimu Majaaliwa kubadili msimamo wa Tumaini kunaonyesha kwamba mwanamke anaweza kushinda vita dhidi ya ukalautala. Momanyi anapinga kauli ya mfumo wa ki-ubabedume wa kumtengea mwanamke majukumu hasi huku mwanamume akihusishwa na yale yenye akili za juu. Tunapata kuiona taswira kamili ya kizazi kipya kinachotambua uwezo wacho na kujiamini kwamba kinaweza.

Mbali na nafasi ambayo mwanamume anachukua katika kumpembeza mwanamke, utamaduni wa jamii unamfanya mwanamke kuwa kizingiti kwa mwanamke mwenzake. Mfumo wa ki-ubabedume unamfanya mwanamke kujidunisha na kujichukulia kama asiyefaa kujitazama vingine mbali na jinsi utamaduni unavyomchukua. Tunamwona Bi. Maimuna akikosa kutambua uwezo wa Tumaini wa kuendeleza masomo na kumpendekezea kuolewa na mwanawe Sifa kabla ya kujiunga na chuo kikuu... '*Unaona aje tukianza kuleta posa....Si vizuri kuwaweka watoto wa kike shuleni kwa muda mrefu. Mtoto wa kike akizeekea*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

*kwao siyo dalili nzuri na huenda vijana wa kiume wakamtilia shaka..*' (uk. 138-139).

Tamaa ya Bi. Maimuna ya kutaka mkazamwana mapema iwezekanavyo inamfanya kutamani ndoa kati ya Tumaini na mwanawe Sifa.. Anathamini ndoa badala ya uwezo wa mwanamke wa kushiriki kwenye ujenzi wa jamii hasa katika uwanja wa kiuchumi. Momanyi ameangazia jinsi mwanamke anavyojitahidi kujikombolea hadhi yake dhidi ya utamaduni dhalilishi kupitia hadithi fupi ya 'Ngome ya Nafsi' (2004) pamoja na *Tumaini* (2007). Amefaulu pakubwa kubainisha uwezo wa mwanamke wa kupigana dhidi ya desturi na mila pembezaji. Mbali na hayo, tunaona sura nyingine ya mwanamke katika utunzaji wa mazingira kama inavyojitokeza katika *Nakuruto* (2010).

**Upembezwaji wa Mwanamke katika Jitihada za Kutunza Mazingira: *Nakuruto* (2010).**

*Nakuruto* (2010) ni riwaya ya Momanyi aliyoiandika baada ya *Tumaini* (2007) na 'Ngome ya Nafsi' (2004). Mwandishi huyu anachukua mtindo wa kifantasia kuonyesha shauku aliyo nayo mwanamke katika ukombozi wa jamii yake kimazingira kiuchumi. Katika jamii za Kiafrika, mwanamke hutengewa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Majukumu hugawanywa kwa msingi wa kijinsia na kiuana ambapo uongozi wa familia hutengewa mwanamume huku mwanamke akiachiwa malezi na utunzaji wa watoto. Mwanamke anatambua kwamba anatengewa nafasi finyu na ndipo Momanyi (2010) anatupa taswira ya mwanake aliyekiuka mipaka aliyowekewa na jamii na kushughulika na ufufuzi wa mazingira.

Nakuruto anapinga kauli kuwa mwanamke ni kiumbe dhaifu kwa kuongoza jamii yake. Anapinga taasubi za kiume zenye mtazamo kuwa maumbile yanampa mwanamke unyonge wa kimwili na kiakili. Nakuruto anajitokeza kama mwanamke aliye na uwezo anaposhughulikia masuala ya kijamii na kimazingira. Ametambua nafasi yake katika jamii na hivyo kushiriki kwenye miradi ya kuikuza jamii yake. Amegundua kuwa, iwapo madhara yatatokea na kurudisha jamii nyuma, ataathirika sawa na wanajamii wengine. Mtazamo huu ndio unamfanya ajaribu kuiokoa jamii yake dhidi ya uchafuzi wa mazingira. Anapofanya hivi, anajijengea ujitambuzinafsia chanya machoni pa wanawake wenzake, wanaume na jamii yake.

Katika kutekeleza jukumu hili, mwandishi anashadidia uwezekano wa jamii kujikomboa katika nyanja za mbalimbali za maisha. Mwanamke anatumiwa katika ufufuzi wa matarajio ya wanajamii kama anavyosema;

> *Nakuruto alimweleza mipango yake ya kuufifisha unyonyaji na kuwarudishia wanakijiji mali zao za asili, ukiwemo ule wa mgodi. Baada ya nasaha nyingi, Mfumwa alikubali shingo upande kwani alijua kuwa asipoungana na wenziwe mambo huenda yakamharibikia*... (uk 66).

Tunaweza kusema kuwa, mwanamke anafaulu kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kujikomboa upya na kuyakomboa mazingira. Mwanamke amejitambua na kujiamini kwamba mchango wake ni mwafaka kwenye ufanisi wa jamii. Mbali na hayo, tunaona kuwa kuna uhusiano kati ya jinsia ya kike na ya kiume katika jamii. Mwanamke na mwanamume kwa pamoja hukamilishana. Mwanamke anaweza kutekeleza majukumu sawa na mwanamume. Momanyi anapinga hoja kwamba mwanamke ni mtawaliwa ilhali mwanamume ni mtawala. Mchango wa Nakuruto unaonyesha uhuru wa kupaaza sauti ya kike pamoja na uhuru wa kimawazo wa mwanamume. Kauli hii inawiana na ya Steady ( 1981, 30-37) anaposema kuwa mwanamke wa Kiafrika anaweza kujitambua na kuikomboa jamii yake.

Mwanamke amekuwa mshiriki kwenye masuala ya jamii yake kwani anaelewa kinachohitajika ili kuiendeleza mbele jamii yake. Anafahamu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Ujitambuzinafsia wake unamfanya kuelewa vyema changamoto zinazoweza kuikumba jamii kutokana na uharibifu wa maliasili zake. Anatoa wosia katika jamii ili kujikinga na hatari kama vile mkurupuko wa magonjwa yanayosababishwa na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

matumizi ya maji machafu. Sauti ya mwanamke inasikika akiizindua jamii kuhusu hoja hii kwa kusema;

> *'chanzo cha mwendelezo wa uhai wenu ni Ipe. Nanyi mko mbioni kuukatiza. Mtoto mchanga akikatiziwa ziwa la mamaye, hatotishiwa uhai wake? Fikiria jibu la swali hili...'?* (uk. 32).

Kupitia kwa mhusika Nakuruto, tunaona mwanamke akishikilia wadhifa wa uongozi. Anatoa onyo la hatari zinazoweza kuikumba jamii nzima kutokana na uharibifu wa mali asili vikiwepo vianzo vya mito inayomwaga maji yake katika Ziwa Ipe. Binadamu anayategemea mali asili kayaimarisha maisha yake. Uharibifu wake unaweza kuyatishia maisha ya vizazi vya sasa na vya baadaye. Inabidi jamii iyatunze mazingira ili kuweza kufaidi mzazao yake ndipo iweze kujiendeleza kimaisha. Uhifadhi wa mazingira ni uhai wa jamii. Kauli ya mhusika Nakuruto inaonyesha jinsi ambavyo mwanamke amejawa na maarifa yanayoweza kuikomboa jamii yake iwapo yatazingatiwa.

Mwanamke anayelengwa na wanaufeministi wa mrengo wa Ubaada wa Usasa wa Ufeministi amefahamikiwa na ukuruba uliopo kati ya uhai wa wanajamii na mazingira yake. Binadamu anaathiriwa moja kwa moja na uharibifu wa mazingira. Mwanamke anailinda jamii yake dhidi ya hatari za uharibifu huu. Kama mlinzi wa jamii, mwanamke anajizatiti kuiokomboa jamii yake. Nafasi anayoichukua na inayowakilishwa na kuwasilishwa na Nakuruto inasawiana na baadhi ya viongozi wa barani Afrika wanaopania kuizindua jamii kuhusu masuala ya kimazingira. Kwa mfano Ameir (2010), anamnukuu makamu wa Rais nchini Tanzania anakiwahutubia wananchi katika Manispaa ya Songea kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira .Makamu huyu wa Rais anahitimisha hotuba yake kwa kusema... '*Tuyatunze mazingira yatutunze...*'. Hivyo, ulimwengu mzima umetambua uhusiano uliopo kati ya mazingira na maisha ya binadamu ulimwenguni. Mwanamke hajaachwa nyuma katika utambuzi huu.

Mbali na kuiongoza jamii katika masuala ya kimazingira, mwanamke amegundua umuhimu wa kuungana kama kundi linalopembezwa na kuijenga jamii katika ngazi ya utawala. Mwanamke amejitambua na kushiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya jamii yake huku akitiwa nguvu na wanawake wenzake. Katika uk. 34, mhusika Bi. Natesha anamtetea Nakuruto kwa kusema kuwa mwanamke anaweza kuwa afisa. Inabainika jinsi ambavyo wanawake wanavyopinga upembezwaji dhidi yao na kutiana nguvu wao kwa wao ili kupaa kwenye ngazi za juu katika uongozi. Anawania nafasi sawa na ya mwanamume katika jamii. Mwanamke anaweza kutekeleza jukumu lolote katika maendeleo ya kijamii ilmuradi atapewa nafasi hiyo.

Mbali na uwezo anaodhihirisha mwanamke katika ujenzi wa jamii, taasubi za kiume zinamfanya kupembezwa na kuchukuliwa kama kiumbe dhaifu na duni. Kila mwaka nchini Kenya katika kituo cha utangazaji cha televesheni ya 'Citizen', kunaangaziwa mwanamke bomba kila siku ya Jumanne. Wanawake mbalimbali wanamulikwa wakitekeleza kazi ambazo kijadi zilitengewa wanaume katika jamii yenye mfumo wa ki-ubabedume. Mfano katika kipindi cha mwezi Julai 24, mwaka 2018 ajuza mwenye uwezo wa kutengeneza redio alipata kuangaziwa. Isitoshe, kuna wanawake wengine kama vile Margaret Vuyewa ambaye ni dereva wa matatu pamoja na Diana Aupe Naker ambaye ni rubani. Awali, kazi wanazozifanya zilitengewa wanaume. Mwanamke amejitambua na kuonyesha uwezo wake wa kushiriki kwenye maendeleo ya jamii yake hasa kiuchumi.

Tunamwona mhusika Sheshije akidhalilishwa anapojitolelea kuupanda mnara wa kupikia nta. Mwanamke anatengwa katika mradi huu. Anakemewa na kukumbushwa kwamba nafasi yake ni nyumbani (uk. 132). Kauli kama hii inakusudiwa kueneza ukalautala katika jamii. Mwanamke hachukuliwi kama kiumbe mwenye uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyotengewa mwanamume. Isitoshe, jamii inamtaraji mwanamke kujitambulisha na mwanamume iwapo anatarajia kutambuliwa kijamii. Mhusika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

Sheshije anavunjwa moyo anapojitahidi kupanda nyenzo ya kuzalisha nta. Aina ya mavazi ya mwanamke inamfanya kukatazwa kupanda. Lazima angevaa kama mwanamume iwapo angeruhusiwa kupanda (uk. 134). Ina maana kwamba ufanisi wa mwanamke unafungamana na wa mwanamume. Dhana hii ni dunifu kwa mwanamke. Jamii inakosa kumwamini na kumshirikisha kikamilifu kwenye miradi ya maendeleo jambo ambalo linaashiria upembezwaji wa hali ya juu dhidi yake.

Katika kufikia ujitambuzinafsia chanya na kupigana na upembezwaji dhidi yake, lazima mwanamke ajiamini na kumwamini mwanamke mwenzake. Mila na desturi ambazo mwanamke hukuzwa kwazo, humfanya kujidunisha na kuhisi kama asiyejiweza. Kupitia kwa mhusika Nakuruto, tunapata taswira ya upinzani dhidi ya uwezo wa mwanamke kando ya ziwa Ipe. Anapowakuta wanawake wakifua nguo hapo ziwani, wengine wao wanamchukulia kama nyapara. Hawaelewi ni vipi mwanamke anavyoweza kuwa afisa wa kukagua ziwa... '*Tangu lini tukawa na maafisa wanawake hapa kwetu? Hicho ni kioja... kwake, wazo la kumhusisha mwanamke na kazi za afisini lilimtia kero kwani hastahili kabisa kutwaa madaraka kama hayo..*. (uk. 33)..Kauli hii inaonyesha kwamba kazi za ofisi ni (za umma) zimetengewa wanaume hivi kwamba mwanamke hafai kupewa vyeo kama hivyo. Mwanamke anapembezwa kwa kutengewa kazi za nyumbani (za faraghani). Utamaduni wa Kiafrika unamsawiri mwanamke kwa unyonge na udhaifu wa kimwili na kiakili. Hii ndiyo sababu inayomfanya mhusika Mama Bintifundi kumdunisha Nakuruto. Anaona kuwa mwanamke hafai kufanya kazi ya ukarani. Tunaweza kuhoji kwamba jamii inamtazama mwanamke kuwili: kama kiumbe mwenye uwezo na kwa upande mmoja na vile vile kama kiumbe dhaifu kwa upande mwingine. Ukinzani huu wa kiitikadi na kimtazamo, unatia doa kubwa katika ujenzi mzima wa ujitambuzinafsia wa mwanamke na jinsia ya kike kwa ujumla.

Mtazamo unaomchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu ni wa kijadi unaowakilishwa na wahusika kama Bintifundi. Hawa wanamchukulia mwanamke kama kiumbe asiyeweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya jamii. Pili, kuna wale wanaomwamini na kumtia shime kupigania nafasi chanya ya ukombozi wa jamii. Hawa wanawakilishwa na mhusika Shisheji. Mtazamo huu hasi unapingwa na mwandishi kwa kuonyesha kwamba mwanamke anaweza kujitambua na kuitumikia jamii yake. Isitoshe, mwanamke ameweza kukaidi ada za jamii kumhusu na kujitokeza kama shujaa. Sifa hii ni dhahiri kupitia kwa mashujaa kama vile Wangari Maathai aliyepata tuzo la Nobeli kwa kutunza mazingira. Mbali na hayo, nchini Kenya tumekuwa na viongozi wanawake waliochaguliwa katika kaunti kama maseneta na magavana. Miongoni mwao ni Kaluki Ngilu (Kitui) na Ann Waiguru (Kirinyaga).

Kwa kuzidi kuangazia nyadhifa za uongozi, tunaona kwamba mwanamke hajaachwa nyuma. Haya ni kwa mujibu wa Kamwara (2016). Anafafanua kuwa kwenye uongozi wa vyuo vikuu nchini Kenya, tumekuwa na Naibu Chansela mwanamke kwa jina Profesa Mugenda (Chuo Kikuu cha Kenyatta). Licha ya hayo, mwanamke anaaminiwa na kuchaguliwa kama kiongozi wa nchi kama jinsi ambavyo Rais Joyce Hilda Banda alivyoliongoza taifa la Malawi kati ya mwaka wa 2012 na 2014. Kupitia kwa viongozi wanawake, tunaweza kudai kuwa mwanamke amejitambua na kushiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya jamii yake. Hayuko tayari kutengewa majukumu duni. Anaweza kutekeleza majukumu ambayo hutengewa mwanamume kwa mujibu wa utamaduni wa jamii za Kiafrika. Hivyo, yeye si kiumbe duni. Isitoshe, wanawake wanashirikiana kama jundi kuinuana na kujengana. Tunaona jisnsi Bi Natesha anavyomtetea Nakuruto kwa kusema kuwa mwanamke anaweza kuwa afisa (uk. 34). Inabainika kwamba mwanamke anapania nafasi za uongozi hasa kwa kutiwa nguvu na kuwezeshwa na jamii kwa jumla.

Kama kiongozi, mwanamke ana uwezo kukabilianna na masuala yanayorudisha jamii nyuma yakiwemo ufisadi, ulafi wa wachache katika jamii unawafanya kutwaa mali ya umma na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

kujifaidi wao wenyewe. Mwanajamii wa kawaida anaachwa huku anateseka. Hali hii inampa mwanamke kiwewe na kuihamasisha jamii yake kuhusu mikakati ya kujikomboa. Kupitia kwa mhusika Nakuruto, tunamwona mwanamke aliyejikomboa kimawazo na kimwili. Anatoa pendekezo mwafaka la kumrejeshea mwanajamii haki yake. Anasema;

> *'Nisikilizeni kwa makini sana. Nina shauku ya kuwapigania nyie na watoto wenu. Sifanyi mzaha. Ninawahakikishia kwamba mkifuata ushauri wangu, bila shaka mtafaulu kumwondoa huyu dhalimu. Chagueni vijana mabarubaru hasa wanaofunuliwa siri ya vilinge vya elimu ya hawa wanguzu ili waweze kupanga mapambano murua...'* (uk. 43).

Mwanamke anapambanua umuhimu wa kuielimisha jamii kuhusu masuala yanayoizunguka. Anamtumia kama mhusika muhimu wa kuipa mwelekeo jamii kuhusu jinsi ya kujipatia ukombozi. Mwanamke ni kiumbe mwenye uwezo wa kuizundua jamii yake. Umahiri wa mwanamke unabainika kupitia mikakati anayopendekeza. Anaelewa umuhimu na uwezo wa elimu ya Kizungu katika kutetea haki za wanajamii. Kupitia kwa mhusika Nakuruto, tunaona jinsi mwanamke alivyofahamikiwa na umuhimu wa kuungana na kupambana na mambo yanayotinga maendeleo katika jamii. Jamii imeanza kujitambulisha na mwanamke kwa kuzingatia mawaidha anayotoa.

## HITIMISHO

Katika kazi za Momanyi ambazo ni '*Ngome ya Nafsi*' (2004), *Tumaini* (2006) na Nakuruto (2010), mwanamke anapembezwa kwa njia anuwai katika jamii. Anahitajika kutimiza mila na desturi za jamii yake ambazo zinamdhil1lisha kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano katika 'Ngome ya Nafsi' pamoja na *Tumaini*, mwanamke anaangaziwa akikumbwa na masaibu katika dunia inayotawaliwa na mwanamume. Hata hivyo, anayatumia masaibu yake kama vuguto la kujikomboa kwa kuivunja ngome ya nafsi yake mwenyewe. Anapigania analohisi linamfaidi kama mtu binafsi mbali na matarajio au ada anazowekewa na jamii. Tumeona kwamba Momanyi amechukua mkondo mpya katika kutunga riwaya ya *Nakuruto* ambapo anamsawiri mwanamke akichukua jukumu la kutunza mazingira na kufanikiwa mbali na upinzani mkali kutoka kwa jamii. Tunaweza kudai kwamba, mazingira ni kiwakilishi cha jinsia ya kike, ni sitiari kuwa yeye ndiye uhai hasa.

## MAREJELEO


Ameir, S. (2010). 'Shein aieleza Afrika: Msidharau Maarifa ya Asilia katika kukabiliana Na changamoto za Mazingira zinazolikabili Bara la Afrika' katika *Jarida la Umaskini na Mazingira.Toleo la* 8:3-4 Penplus Ltd: Tanzania.

Chesaina, C. (1987). *Women in African Drama: Representation and Role* (Doctoral dissertation, University of Leeds).

Eagleton, M. (1991). *Feminist Literary Criticism - Woman in Literature*. London: Longhorn Publisher.

Lugano, R. S. (1989). *Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi*. Gainesville: Florida University Press.

Kamwara, K. (2016). 'Mtazamo Mpya katika Sauti ya Kike katika Riwaya ya Kiswahili'. *Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Mount Kenya. (Haijachapishwa).*

Mavisi, R. (2007). 'Usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Z. Burhani'. *Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mikell, G., (1997). *African Feminism: The Politics of Survival in Sub-Sahara Africa*. University of Pennsylvania Press Mohamed, S.A. (1980), *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mogere, O. (2003). 'Uhakiki wa riwaya za Said Ahmed Mohamed katika misingi ya Kiufeministi'. *Tasnifu ya Uzamili. Chuo*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1978

*Kikuu cha Nairobi*. *(*Haijachapishwa)Momanyi, C.

(1998). 'Usawiri wa Mwanamke Mwislimu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili'. *Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)*

Mohamed, S.A. (1980), *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers

Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Nairobi: Vide – Muwa publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi: Longhorn publishers.

Muindi, A. (1990). Usawiri wa Wahusika Makahaba Katika Riwaya za S.A Mohamed. *Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.*

Musyoka F.M. (2011). 'An Analysis of the Women in Gender Role-Play Dyanamics in Kenyan Kiswahili Drama.' (Doctoral dissertation, University of Nairobi, Kenya).

Mwanahamisi, H. (2018, 24 Julai) Mwanamke Bomba. *Msururu wa Vipindi vya Televisheni ya Citizen Kenya*. https://youtu.be/WvlnJgnPyVo

Ndungo, C. (1998). Images of Women as Exemplified in Gikuyu and Swahili Proverbs. *Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).*

Nkealah, N. (2006) 'Conceptualizing Feminism in Africa. The challenges facing African Women writers and Critics. English Academy Review, 23:1, 133-144 DOI:10.1080/10131750608540431'

Pinkie, M., (2006). Theorizing African Feminism(s): The Colonial Question. *QUEST: An African journal of Philosophy, 20(1-2)*, 11-22.

Steady, F. C. (1981). *Reflecting on the Politics of Sisterhood*. New York: African Wordpress.

Swaleh, A. (2011). *A critique of the mapping and construction of gender identity and authority in selected Kiswahili novels* (Doctoral dissertation, University of Nairobi, Kenya).

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Focus Publishers.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.